SAUTI YA TSC

TOLEO NA. 69 JARIDA LA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU TANZANIA (TSC) NOVEMBA 2026

BARAZA LA WAFANYAKAZI TSC LAPITIA UTEKELEZAJI WA BAJETI NA MAJUKUMU YA TUME



Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi la Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) akifungua rasmi Mkutano Na. 1/2026/2027 wa Baraza hilo, uliofanyika tarehe 5 Novemba 2026 katika Ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete, jijini Dodoma.

MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz

Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania tumeyautumishiwawalimutanzania

KONGOLE WALIMU WETU KWA ONGEZEKO LA UFAULU WA WANAFUNZI WA DARASA LA SABA MWAKA 2026

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) inawapongeza walimu wote nchini kwa mchango wao mkubwa katika kuongeza kiwango cha ufaulu wa Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi kwa mwaka 2026. Mafanikio haya yanaonesha juhudi, kujituma na uwajibikaji wa walimu katika kutekeleza jukumu lao la msingi la kufundisha, kuongoza na kuwaandaa wanafunzi kupata maarifa na ujuzi unaohitajika katika maisha yao.

Kwa mujibu wa matokeo yaliyotangazwa na Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA) tarehe 3 Novemba 2026, ufaulu wa jumla umefikia asilimia 85.22, sawa na watahiniwa 970,876 kati ya 1,139,273 waliofanya mtihani na kuwa na matokeo. Kiwango hicho ni ongezeko la asilimia 3.42 ikilinganishwa na asilimia 81.80 ya mwaka 2025. Aidha, watahiniwa 429,667, sawa na asilimia 37.72, wamepata madaraja ya A na B. Takwimu hizi ni ishara ya maendeleo yanayopaswa kutambuliwa na kuungwa mkono.

TSC inatambua kuwa mafanikio haya ni matokeo ya juhudi za pamoja za walimu, viongozi wa shule, wazazi, Serikali na wadau wengine wa elimu. Hata hivyo, walimu wana nafasi ya kipekee katika mafanikio hayo kutokana na mchango wao katika kufundisha na kusimamia maendeleo ya wanafunzi.

Katika kuunga mkono juhudi hizo, TSC itaendelea kuboresha na kutoa huduma bora kwa walimu kwa wakati, kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma. Tume inaamini kuwa walimu wanapopata huduma stahiki na mazingira bora ya kiutumishi, huongezeka ari na uwezo wao wa kutekeleza majukumu kwa ufanisi.

Pamoja na pongezi hizi, TSC inawahimiza walimu kuendelea kujituma, kuzingatia weledi na ubunifu katika ufundishaji ili mafanikio haya yawe endelevu na yaende sambamba na ubora wa elimu. Tume pia inatoa wito kwa wazazi, walezi na wadau wengine kuendelea kushirikiana na walimu katika kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji. Kwa pamoja, tunaweza kujenga mfumo imara wa elimu utakaowezesha kupata wataalamu wenye maarifa, ujuzi na uwezo wa kuchangia maendeleo ya Taifa.

KATUNI



BODI YA UHARIRI

Mwenyekiti
Paulina M. Nkwama

Wajumbe
Revocatus P. Misonge
Mectildis F. Kapinga
Lameck S. Mbeya
Zachary A. Dida
Fatuma I. Muya
Edwin Mgendera
Asha Lubuva

Mhariri Mkuu
Artemony T. Vincent

Mhariri
Adili J. Mhina

Msanifu Kurasa
Lucas G. Ogunde

BARAZA LA WAFANYAKAZI TSC LAPITIA UTEKELEZAJI WA BAJETI NA MAJUKUMU YA TUME

Na Mwandishi – Dodoma.

Baraza la Wafanyakazi la Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) limekutana kujadili na kupitia utekelezaji wa bajeti na majukumu ya Tume kwa mwaka wa fedha 2025/2026, pamoja na utekelezaji wa majukumu kwa kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2026/2027, Julai hadi Septemba 2026.

Mkutano huo Na. 1/2026/2027 umefanyika tarehe 5 Novemba 2026 katika Ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete, jijini Dodoma, ukilenga kupitia mafanikio yaliyopatikana, changamoto zilizojitokeza na kuweka mikakati ya kuboresha utekelezaji wa majukumu ya Tume.

Akifungua mkutano huo, Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi, Mwl. Paulina Nkwama aliwataka wajumbe kushiriki kikamilifu katika majadiliano na kutoa maoni yenye kujenga kwa niaba ya watumishi wanaowawakilisha.

Mwl. Nkwama alifafanua kuwa Baraza ni jukwaa muhimu la kuimarisha ushirikiano kati ya Menejimenti na wafanyakazi, kujadili changamoto na kuweka mikakati ya kuboresha utendaji na mazingira ya kazi.

Katika neno la utangulizi, Katibu wa Baraza la Wafanyakazi, Bw. Nuhu Mlekwa, alieleza kuwa mikutano ya Baraza inatoa fursa kwa wajumbe kupitia utekelezaji wa bajeti na mipango ya Taasisi, kujadili masuala ya ustawi wa wafanyakazi na kutoa mapendekezo yanayolenga kuboresha utendaji wa Tume.

Pamoja na mambo mengine, wajumbe wa mkutano huo walipitia taarifa za utekelezaji wa majukumu ya Tume kwa mwaka wa fedha 2025/2026 na kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2026/2027.

Baada ya kupokea taarifa hizo, wajumbe walijadili na kutoa mapendekezo mbalimbali yaliyolenga kuboresha mipango na utekelezaji wa majukumu ya Tume, kuimarisha matumizi bora ya rasilimali za umma na kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma kwa walimu na wadau wengine wa sekta ya elimu.

Aidha, ikiwa ni sehemu ya mkakati wa Tume wa kuimarisha afya na ustawi wa watumishi na kukabiliana na magonjwa sugu yasiyoambukiza, washiriki walipatiwa elimu kuhusu lishe bora na Afisa Lishe kutoka Hospitali ya Benjamin Mkapa, Bi. Jane P. Ndanga. Elimu hiyo ililenga kuwajengea watumishi uelewa kuhusu umuhimu wa kuzingatia lishe bora katika kulinda afya zao.

Mkutano huo umehitimishwa kwa kusisitiza umuhimu wa uwazi, uwajibikaji, nidhamu na ushirikiano katika utekelezaji wa majukumu ya Tume. Wajumbe pia wamehimizwa kuhakikisha maoni na mapendekezo yanayotolewa katika Baraza yanazingatiwa na kufanyiwa kazi ili kuleta maboresho katika utendaji wa Taasisi na utoaji wa huduma bora kwa walimu nchini.



Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi la Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) akifungua rasmi Mkutano Na. 1/2026/2027 wa Baraza hilo, uliofanyika tarehe 5 Novemba 2026 katika Ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete, jijini Dodoma.



Katibu wa Baraza la Wafanyakazi la TSC, Bw. Nuhu Mlekwa, akitoa neno la ukaribisho wakati wa ufunguzi wa mkutano wa Baraza hilo jijini Dodoma.

BARAZA LA WAFANYAKAZI TSC LAPITIA UTEKELEZAJI WA BAJETI NA MAJUKUMU YA TUME



Afisa Lishe kutoka Hospitali ya Benjamin Mkapa, Bi. Jane P. Ndanga, akitoa elimu kuhusu lishe bora kwa watumishi wa TSC ikiwa ni sehemu ya mkakati wa Tume wa kukabiliana na magonjwa sugu yasiyoambukiza katika Mkutano Na. 1/2026/2027 wa Baraza la Wafanyakazi la TSC uliofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete, jijini Dodoma.









Washiriki wa Mkutano Na. 1/2026/2027 wa Baraza la Wafanyakazi la TSC wakiwa kwenye kikao kilichofanyika tarehe 5 Novemba 2026 katika Ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete, jijini Dodoma.

BARAZA LA WAFANYAKAZI TSC LAPITIA UTEKELEZAJI WA BAJETI NA MAJUKUMU YA TUME













Washiriki wa Mkutano Na. 1/2026/2027 wa Baraza la Wafanyakazi la TSC wakiwa kwenye kikao kilichofanyika tarehe 5 Novemba 2026 katika Ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete, jijini Dodoma.

BARAZA LA WAFANYAKAZI TSC LAPITIA UTEKELEZAJI WA BAJETI NA MAJUKUMU YA TUME



Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Nkwama (katikati kwa waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya washiriki wa Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi uliofanyika tarehe 5 Novemba, 2026 katika Ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete, jijini Dodoma.

BARAZA LA WAFANYAKAZI TSC LAPITIA UTEKELEZAJI WA BAJETI NA MAJUKUMU YA TUME

















Washiriki wa Mkutano Na. 1/2026/2027 wa Baraza la Wafanyakazi la TSC wakiwa kwenye kikao kilichofanyika tarehe 5 Novemba 2026 katika Ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete, jijini Dodoma.

BARAZA LA WAFANYAKAZI TSC LAPITIA UTEKELEZAJI WA BAJETI NA MAJUKUMU YA TUME












Washiriki wa Mkutano Na. 1/2026/2027 wa Baraza la Wafanyakazi la TSC wakiwa kwenye kikao kilichofanyika tarehe 5 Novemba 2026 katika Ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete, jijini Dodoma.

BARAZA LA WAFANYAKAZI TSC LAPITIA UTEKELEZAJI WA BAJETI NA MAJUKUMU YA TUME











Washiriki wa Mkutano Na. 1/2026/2027 wa Baraza la Wafanyakazi la TSC wakiwa kwenye kikao kilichofanyika tarehe 5 Novemba 2026 katika Ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete, jijini Dodoma.

OLIVER MHAIKI: SAFARI YA KUJENGA TSC YA SASA





Mwenyekiti wa Kwanza wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) akiwa katika mahojiano maalum na jarida la Sauti ya TSC.

Na Mwandishi Wetu – Dodoma

Kuanzisha taasisi mpya ya umma kunahitaji zaidi ya uteuzi wa viongozi na ugawaji wa majukumu. Kunahitaji kuweka mifumo imara ya utendaji, kujenga uratibu kati ya ngazi mbalimbali za uongozi na kuhakikisha huduma zinaendelea kutolewa kwa wananchi. Hiyo ndiyo safari aliyopitia Oliver Mhaiki, Mwenyekiti wa kwanza wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), aliyeteuliwa na Rais wa Awamu ya Tano, Dkt. John Pombe Magufuli, na kuiongoza Tume kuanzia mwaka 2016 hadi 2019.

Alipoanza uongozi wake, Mhaiki alikabiliwa na jukumu la kusaidia kuiweka Tume katika misingi imara ya kiutendaji, huku akihakikisha kuwa mabadiliko ya kiutawala hayaathiri utoaji wa huduma kwa walimu. Ingawa alikuwa na uzoefu wa uongozi katika taasisi mbalimbali za Umma na alifahamu masuala ya nidhamu, kufanya kazi katika taasisi mpya yenye majukumu mahususi ya kusimamia utumishi wa walimu kulihitaji kujifunza na kuzoea mazingira mapya.

"Kipindi cha mwanzo kilihitaji umakini mkubwa, hasa kwa sababu tulikuwa katika kipindi cha mpito. Tulipaswa kuhakikisha kuwa mabadiliko hayo hayaathiri utoaji wa huduma, wakati viongozi wote walikuwa wapya na taasisi yenyewe ilikuwa mpya," anakumbuka Mhaiki.

Kuweka Misingi ya Utendaji

Moja ya vipaumbele vya uongozi wake ilikuwa kuhakikisha kuwa Tume inaweka mgawanyo wa majukumu kwa kuzingatia sheria na kuimarisha uratibu wa kazi kati ya Makao Makuu na ofisi za wilaya. Aidha, ilihitajika kuweka uhusiano mzuri wa kiutendaji na waajiri wa walimu ili masuala ya utumishi yashughulikiwe kwa kufuata taratibu zilizowekwa.

Jambo jingine muhimu lilikuwa kuhakikisha walimu wanaelewa namna ya kuwasilisha malalamiko, rufaa na masuala mengine yanayohusu utumishi wao. Kwa Mhaiki, mifumo hiyo ilikuwa muhimu katika kuweka utaratibu unaoeleweka wa kushughulikia changamoto za walimu na kuwezesha Tume kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Hata hivyo, kazi hiyo ilifanyika katika mazingira yenye changamoto za rasilimali. Tume ilikabiliwa na upungufu wa fedha na vitendea kazi, hali iliyofanya isiwezekane kutekeleza mipango yote kwa wakati mmoja. Hivyo, uongozi ulilazimika kuweka vipaumbele na kutekeleza baadhi ya mipango hatua kwa hatua.

Miongoni mwa mipango iliyohitaji muda na maandalizi zaidi ilikuwa kuweka majalada ya walimu katika mfumo wa kidijitali. Kwa mujibu wa Mhaiki, Tume ilitamani kuwa na kumbukumbu za walimu zilizohifadhiwa kidijitali ili kurahisisha upatikanaji na usimamizi wa taarifa zao, lakini uhaba wa rasilimali ulifanya mpango huo uhitaji muda zaidi wa utekelezaji.

Changamoto hizo zilimfundisha kuwa kujenga taasisi mpya kunahitaji uvumilivu, kujifunza na kutumia rasilimali zilizopo kwa kuzingatia vipaumbele vya huduma.

Nidhamu ya Walimu: Kati ya Sheria na Uelewa

Mbali na kujenga mifumo ya kiutendaji, Mhaiki alikumbana na changamoto ya mashauri mengi ya kinidhamu yaliyohusiana kwa kiasi fulani na uelewa mdogo wa baadhi ya walimu kuhusu sheria, kanuni na taratibu za utumishi wao.

Katika kipindi hicho, Tume ilipokea rufaa kutoka kwa walimu ambao mashauri yao yalikuwa yameshughulikiwa katika ngazi za wilaya. Mhaiki anakumbuka kuwa baadhi ya walimu walikuwa

OLIVER MHAIKI: SAFARI YA KUJENGA TSC YA SASA



Mwenyekiti wa Kwanza wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) akiwa katika mahojiano maalum na jarida la Sauti ya TSC.

na uelewa mzuri wa sheria na taratibu, lakini wengine walionesha kutofahamu makosa waliyokuwa wamefanya au taratibu walizopaswa kufuata.

Hali hiyo iliweka wazi umuhimu wa kutoa elimu kwa walimu kuhusu haki zao, wajibu wao na matokeo ya kutofuata taratibu za utumishi. Kwa hiyo, jukumu la Tume halikuwa kushughulikia mashauri yaliyowasilishwa pekee, bali pia kuongeza uelewa wa walimu ili kusaidia kuzuia makosa ya kinidhamu.

Miongoni mwa makosa yaliyojitokeza mara kwa mara ilikuwa ni utoro kazini. Baadhi ya walimu walikwenda masomoni bila kupata ruhusa ya mwajiri, huku wengine wakikaa nyumbani wanapougua bila kutoa taarifa zinazohitajika. Mhaiki anasema baadhi yao hawakuzifahamu taratibu, wakati wengine walizifahamu lakini hawakuzifuata.

Changamoto hizo zilionesha kuwa usimamizi wa nidhamu unahitaji zaidi ya hatua za kinidhamu. Unahitaji pia elimu endelevu, ufuatiliaji na uwajibikaji ili walimu watambue umuhimu wa kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia sheria na taratibu za utumishi.

Mashauri Nyeti Yaliyohitaji Umakini

Miongoni mwa mashauri yaliyokuwa magumu kushughulikia ni yale yaliyohusu madai ya mahusiano ya kimapenzi kati ya walimu na wanafunzi. Kwa mujibu wa Mhaiki, wakati mwingine ilikuwa vigumu kupata ushahidi, hasa pale mwanafunzi alipoulizwa kuhusu tukio linalodaiwa na kukataa kuwa lilitokea.

Mashauri ya aina hiyo yalihitaji umakini mkubwa katika uchunguzi na tathmini ya ushahidi. Yaliweka wazi umuhimu wa kufuata taratibu zinazotumika katika kushughulikia mashauri ya kinidhamu na kuhakikisha kuwa maamuzi yanafanywa kwa kuzingatia ushahidi uliopo.

Kuendeleza Safari ya Tume

Mhaiki anasema alitekeleza majukumu yake kwa ushirikiano na viongozi pamoja na watumishi wa Tume, ambao walimsaidia kujifunza na kupata uzoefu katika kipindi chake cha uongozi. Anaishukuru Serikali kwa kumwamini na kumpa nafasi ya kuongoza taasisi yenye jukumu muhimu la kutoa huduma kwa walimu.

Baada ya kumaliza muda wake mwaka 2019, nafasi yake ilichukuliwa na Profesa Willy Komba, ambaye Mhaiki anamtaja kuwa kiongozi mwenye uzoefu mkubwa katika sekta ya elimu na aliyefanya vizuri katika kipindi chake cha uongozi.

Kwa Mhaiki, kuiongoza Tume katika miaka yake ya mwanzo ilikuwa fursa ya kipekee ya kujifunza na kushiriki katika kujenga taasisi mpya. Changamoto za rasilimali, kuweka mifumo ya utendaji, kuimarisha uratibu na kushughulikia mashauri ya kinidhamu zilikuwa sehemu ya safari hiyo.

Katika kuadhimisha miaka 10 ya Tume ya Utumishi wa Walimu, uzoefu wake unaweka kumbukumbu ya majukumu na changamoto zilizokuwepo katika hatua za mwanzo za Tume. Pia unaonesha umuhimu wa kuwa na mifumo inayoeleweka, watumishi wenye uelewa wa sheria na taratibu, pamoja na rasilimali zinazowezesha huduma kutolewa kwa ufanisi.

Safari ya Mhaiki inakumbusha kuwa kujenga taasisi ni mchakato unaohitaji muda, ushirikiano na kujifunza kutokana na changamoto. Misingi ya utendaji inayowekwa katika hatua za mwanzo ni sehemu muhimu ya safari ya taasisi kuelekea utoaji bora wa huduma kwa wananchi.

TSC mbioni kuandaa kanuni mpya za kuboresha huduma kwa walimu

Na Mwandishi Wetu – Morogoro

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) inaendelea kukusanya maoni ya wadau kwa ajili ya kuandaa kanuni mpya zitakazoimarisha utendaji wa Tume na kuboresha huduma zinazotolewa kwa walimu nchini.

Akizungumza na washiriki wa kikao kazi cha kupokea maoni kuhusu Kanuni mpya za Tume tarehe 21 Oktoba 2026, Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama alisema mchango wa wadau ni muhimu katika kuhakikisha kanuni zitakazoandaliwa zinazingatia mahitaji ya sasa na matarajio ya walimu.

Nkwama alisema ushiriki wa wadau mbalimbali katika kazi hiyo utawapa nafasi ya kuifahamu Tume na majukumu yake kwa karibu huku wakichangia moja kwa moja katika kuandaa kanuni zitakazosaidia kuongeza ufanisi wa huduma kwa walimu.

"Lengo kubwa ni kuhakikisha mwalimu anapata huduma bora zaidi," alisema.

Aliwataka washiriki kutekeleza jukumu hilo kwa uadilifu, uaminifu na bidii huku akisema kuwa Serikali imewaamini katika mchakato huo. Aliongeza kuwa maoni yatakayokusanywa yataisaidia Tume kuandaa kanuni zinazozingatia mazingira ya sasa na kuimarisha huduma kwa walimu.

Kwa upande wake mshiriki wa kikao hicho, Bw. Sylvester Kabamba, Afisa Sheria kutoka Halmashauri ya Jiji la Tanga aliishukuru Tume kwa kuwashirikisha wadau. Alisema washiriki watautekeleza wajibu huo kwa weledi ili kusaidia kupatikana kwa kanuni bora zinazokidhi mahitaji ya sasa.

Kikao kazi cha kupokea maoni hayo kinafanyika mjini Morogoro kuanzia Oktoba 20 hadi 23, 2026. Kimewashirikisha wataalamu wa sheria, elimu na rasilimaliwatu kutoka ofisi mbalimbali za Serikali.





Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Nkwama akizungumza na washiriki wa kikao kazi cha kupokea maoni kuhusu Kanuni mpya za Tume mjini Morogoro tarehe 21 Oktoba 2026.





Mkurugenzi wa Kitengo cha Huduma za Sheria wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Bw. Edwin Mgendera akitoa neno la kumkaribisha Katibu wa Tume wakati wa kikao kazi cha kupokea maoni kuhusu Kanuni mpya za Tume mjini Morogoro tarehe 21 Oktoba 2026.

TSC mbioni kuandaa kanuni mpya za kuboresha huduma kwa walimu





Mkurugenzi Msaidizi wa Sehemu ya Usimamizi wa Rasilimaliwatu Tume ya Utumishi wa Walimu, Bw. Salvatory Kaiza, akitoa neno la utangulizi wakati wa kikao kazi cha kupokea maoni kuhusu Kanuni mpya za Tume mjini Morogoro tarehe 21 Oktoba 2026.



Afisa Sheria kutoka Halmashauri ya Jiji la Tanga, Bw. Sylvester Kabamba akitoa neno la shukrani kwa Katibu wa Tume (hayupo pichani) wakati wa kikao kazi cha kupokea maoni kuhusu Kanuni mpya za Tume mjini Morogoro tarehe 21 Oktoba 2026.







Washiriki wa kikao kazi cha kupokea maoni kuhusu Kanuni mpya za Tume wakiwa kwenye kikao hicho mjini Morogoro, tarehe 21 Oktoba 2026.

TSC mbioni kuandaa kanuni mpya za kuboresha huduma kwa walimu











Washiriki wa kikao kazi cha kupokea maoni kuhusu Kanuni mpya za Tume wakiwa kwenye kikao hicho mjini Morogoro, tarehe 21 Oktoba 2026.

Na Mwandishi wetu – Dar es Salaam.

LETISIA AUGUSTINE: SAFARI YA MIAKA 23 KATIKA KUWAHUDUMIA WALIMU



Mwl. Letisia Augustine akizungumza na Jarida la Sauti ya TSC hivi karibuni.

Kwa Letisia Andrew Augustine, aliyestaafu utumishi mwaka 2014 akiwa na umri wa miaka 60, historia ya usimamizi wa utumishi wa walimu nchini si jambo la kusimuliwa tu, bali ni sehemu ya maisha yake ya kazi. Alianza kuitumikia Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) mwaka 1991, akishiriki katika majukumu yaliyohusu maslahi, ajira na maendeleo ya walimu.

Alipoanza kazi, alipangiwa Kitengo cha Pensheni na Mirathi, ambako jukumu lake kuu lilikuwa kukokotoa mafao ya pensheni kwa walimu waliostaafu pamoja na masuala ya mirathi. Kwa kipindi hicho, umri wa kustaafu kwa lazima ulikuwa miaka 55, huku mwalimu akiruhusiwa kustaafu kwa hiari akiwa na umri wa miaka 50, kwa mujibu wa taratibu zilizokuwepo wakati huo.

Alitumia miaka mitano katika kitengo hicho, akishughulikia masuala yaliyogusa moja kwa moja maslahi ya walimu baada ya utumishi. Baadaye, alihamishiwa Kitengo cha Ajira na Maendeleo ya Walimu, hatua iliyompa fursa ya kushiriki katika masuala mapana zaidi ya usimamizi wa utumishi wa walimu.

Elimu kwa Walimu: Njia ya Kuzuia Ukiukwaji wa Maadili

Mbali na majukumu ya kiutawala, mojawapo ya shughuli alizozikumbuka ni kutoa elimu kwa walimu kuhusu taratibu za ajira, nidhamu na pensheni. Timu yao ilitembelea maeneo mbalimbali kukutana na walimu na kuwaeleza haki zao, wajibu wao na taratibu walizopaswa kufuata katika utumishi.

Elimu hiyo haikuishia kwa walimu waliokuwa tayari kazini. Katika baadhi ya vipindi, walitembelea vyuo vilivyokuwa vikitoa mafunzo ya ualimu ili kukutana na wanafunzi waliokuwa wakijiandaa kuingia katika taaluma hiyo. Lengo lilikuwa kuwajengea uelewa wa mapema kuhusu taratibu za utumishi na maadili yanayotakiwa kwa mwalimu.

Kwa mujibu wa Letisia, juhudi hizo zilisaidia kupunguza kwa kiwango kikubwa kesi za ukiukwaji wa maadili ya ualimu. Hili linaonesha umuhimu wa kutoa elimu ya kinga kabla changamoto za kinidhamu hazijatokea, badala ya kusubiri makosa yatendeke ndipo hatua zichukuliwe.

Uzoefu wake unasisitiza kuwa usimamizi bora wa utumishi wa walimu hauishii katika kushughulikia ajira na nidhamu pekee. Pia unahitaji kuwawezesha walimu kuelewa wajibu wao wa kitaaluma na kuwajengea msingi wa kufanya maamuzi sahihi katika mazingira ya kazi.

Kutoka TSC ya Zamani hadi TSD

Katika safari yake ya utumishi, Letisia alishuhudia mabadiliko ya kiutawala yaliyohusisha Tume ya Utumishi wa Walimu ya zamani na Idara ya Huduma za Walimu (TSD), iliyokuwa chini ya Utumishi wa Umma. Kwa mujibu wa kumbukumbu yake, licha ya mabadiliko hayo ya kiutawala, majukumu yao ya msingi yaliendelea kuhusisha masuala ya ajira, nidhamu na maslahi ya walimu.

Akiitazama safari yake kwa ujumla, anasema anashukuru Mungu kwa kuwa walitekeleza majukumu yao vizuri. Kauli hiyo inaakisi kuridhika kwake na huduma aliyotoa katika kipindi chote alichokuwa mtumishi wa umma.

Uzoefu wa Letisia ni sehemu ya historia pana ya usimamizi wa utumishi wa walimu nchini. Katika kuadhimisha miaka 10 ya Tume ya Utumishi wa Walimu tangu kuanzishwa kwake upya mwaka 2016, simulizi yake inatoa fursa ya kutafakari majukumu yaliyotekelezwa katika vipindi tofauti na umuhimu wa kuendelea kuboresha huduma kwa walimu.

Wito kwa Serikali: Walimu Wawezeshwe Kukabiliana na Mabadiliko

Licha ya kustaafu kwake, Letisia anaendelea kufuatilia mahitaji ya walimu na mabadiliko yanayoikabili sekta ya elimu. Wito wake kwa Serikali ni kuendelea kuwaangalia walimu kwa jicho la pekee, hasa kwa kuboresha mazingira wanamofanyia kazi na kuwapatia vitendea kazi vinavyorahisisha utekelezaji wa majukumu yao.

Aidha, anasisitiza umuhimu wa kuwawezesha walimu kupata elimu na ujuzi unaoendana na maendeleo ya teknolojia. Anaamini kuwa maandalizi hayo ni muhimu ili walimu waweze kukabiliana na mabadiliko ya mifumo ya ufundishaji na mitaala, na hatimaye kutoa elimu inayokidhi mahitaji ya maendeleo ya Taifa.

Kwa mtazamo wake, uwekezaji kwa walimu haupaswi kuishia katika ajira pekee, bali unapaswa kuhusisha pia mazingira bora ya kazi, upatikanaji wa vitendea kazi na mafunzo endelevu. Haya ni mambo muhimu katika kuhakikisha kuwa walimu wana uwezo wa kutekeleza wajibu wao kwa ufanisi katika mazingira ya elimu yanayoendelea kubadilika.

SERIKALI YALIPA STAHIKI ZA WALIMU 1,822 SUMBAWANGA ZAIDI YA SHILINGI BILIONI MOJA

Na Mwandishi Wetu, Sumbawanga

Serikali imelipa zaidi ya shilingi bilioni moja za stahiki mbalimbali kwa walimu 1,822 katika Manispaa ya Sumbawanga, mkoani Rukwa, katika kipindi cha mwaka 2023 hadi 2026, ikiwa ni sehemu ya jitihada za kutatua changamoto zinazowakabili walimu na kuboresha mazingira ya utendaji kazi.

Hayo yameelezwa na Afisa Elimu wa Manispaa ya Sumbawanga, Bw. Musa Ernest Musoma, wakati wa mahojiano na Afisa wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini kutoka Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), yaliyolenga kueleza mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita katika kutatua changamoto za walimu.

Bw. Musoma alisema kuwa katika kipindi hicho, Serikali imelipa stahiki za walimu zilizohusisha fedha za likizo, gharama za uhamisho na malimbikizo ya mishahara, hatua iliyosaidia kupunguza madai ya walimu na kuboresha ustawi wao.

Alifafanua kuwa jumla ya shilingi milioni 485.8 zimelipwa kwa walimu 1,375 kama fedha za likizo, huku shilingi milioni 269.2 zikilipwa kwa walimu 113 waliohamishwa vituo vyao vya kazi.

Aidha, alisema kuwa katika kipindi cha mwaka 2023 hadi 2026, walimu 334 walilipwa malimbikizo ya mishahara yenye jumla ya shilingi milioni 272.4.

Kwa ujumla, malipo hayo yana thamani ya shilingi bilioni 1.0274, sawa na zaidi ya shilingi bilioni moja, kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa.

Katika hatua nyingine, Bw. Musoma alisema kuwa Manispaa hiyo inaendelea kuchukua hatua za kuimarisha taaluma ya ualimu kwa kutoa fursa za kujiendeleza kielimu na mafunzo kazini, ili kuongeza maarifa na ujuzi wa walimu na kuboresha ufundishaji na ujifunzaji.

Alisema kuwa katika kipindi cha mwaka 2024 hadi 2026, jumla ya walimu 46 walipata ruhusa ya kwenda masomoni kwa lengo la kuongeza ujuzi na kuboresha uwezo wao wa kitaaluma.

Aliongeza kuwa kuanzia mwaka 2023 hadi 2026, walimu 474 walipatiwa mafunzo kazini yaliyolenga kuwaongezea maarifa, ujuzi na stadi za kuwasaidia kuboresha ufundishaji na kuwaandaa wanafunzi kukabiliana na mahitaji ya soko la ajira na maisha kwa ujumla.

Akizungumzia matumizi ya teknolojia katika elimu, Bw. Musoma alisema kuwa Manispaa hiyo imegawa vifaa vya kielektroniki katika shule tatu za msingi ili kuimarisha matumizi ya teknolojia katika ufundishaji na ujifunzaji.

Alivitaja vifaa hivyo kuwa ni kompyuta 60, mashine tatu za kudurufu na mbao tatu za kisasa za kielektroniki (smart boards), ambazo zinatarajiwa kusaidia kuboresha upatikanaji wa maarifa na matumizi ya teknolojia katika mazingira ya shule.

Alisisitiza kuwa juhudi za kulipa stahiki za walimu, kuwaendeleza kitaaluma na kuboresha upatikanaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia ni muhimu katika kuimarisha ubora wa elimu na kuunga mkono utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2050.



Afisa Elimu wa Manispaa ya Sumbawanga, Bw. Musa Ernest Musoma, akifafanua mafanikio ya Serikali katika kutatua changamoto za walimu wakati wa mahojiano na Afisa wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini kutoka Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Makao Makuu, ofisini kwake hivi karibuni.





Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama, akizungumza na washiriki wa kikao kazi cha kushughulikia masuala ya rasilimali watu ya Tume, kilichofanyika tarehe 27 Oktoba 2026, mjini Morogoro.



Mkurugenzi Msaidizi wa Sehemu ya Utawala wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Bi. Josephine Duway, akitoa neno la ukaribisho kwa Katibu wa Tume wakati wa kikao kazi cha kushughulikia masuala ya rasilimali watu ya Tume, kilichofanyika tarehe 27 Oktoba, 2026 mjini Morogoro.



Mkurugenzi Msaidizi wa Sehemu ya Usimamizi wa Rasilimaliwat Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Bw. Salvatory Kaizer, akitoa neno la utangulizi wakati wa kikao kazi cha kushughulikia masuala ya rasilimali watu ya Tume, kilichofanyika tarehe 27 Oktoba, 2026 mjini Morogoro.







Washiriki wa kikao kazi cha kushughulikia masuala ya rasilimali watu ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) wakiwa kwenye kikao kazi hicho kilichofanyika tarehe 27 Oktoba 2026, mjini Morogoro.













Washiriki wa kikao kazi cha kushughulikia masuala ya rasilimali watu ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) wakiwa kwenye kikao kazi hicho kilichofanyika tarehe 27 Oktoba 2026, mjini Morogoro.

TSC NKASI YAPANDISHA VYEO WALIMU 1,193, KUIMARISHA MORALE NA UFANISI KAZINI

Na Mwandishi Wetu, Nkasi

Jumla ya walimu 1,193 katika Wilaya ya Nkasi, Mkoa wa Rukwa, wamepandishwa vyeo katika kipindi cha miaka mitatu kuanzia mwaka 2023 hadi 2026, hatua iliyolenga kutambua utumishi wao, kuongeza ari ya kazi na kuimarisha ufanisi katika ufundishaji na ujifunzaji.

Hayo yameelezwa na Kaimu Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Nkasi, Bw. Richard M. Katyega, wakati wa mahojiano na Maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini kutoka Makao Makuu ya Tume, Dodoma, yaliyolenga kueleza mafanikio ya Tume katika kipindi cha miaka 10 tangu kuanzishwa kwake.

Akifafanua kuhusu utekelezaji wa upandishaji wa vyeo, Bw. Katyega alisema kuwa katika kipindi cha mwaka 2023/2024, walimu 771 walipandishwa vyeo, wakiwemo 598 wa shule za msingi na 173 wa shule za sekondari.



Kaimu Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Nkasi, Bw. Richard M. Katyega, akifafanua masuala mbalimbali kuhusu mafanikio ya Tume wakati wa mahojiano na Maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini kutoka Makao Makuu ya Tume, Dodoma.

Aliongeza kuwa katika mwaka 2024/2025, walimu 116 walipandishwa vyeo, wakiwemo 67 wa shule za msingi na 49 wa shule za sekondari. Aidha, katika mwaka 2025/2026, walimu 306 walipandishwa vyeo, wakiwemo 230 wa shule za msingi na 76 wa shule za sekondari.

Kwa mujibu wa Bw. Katyega, hatua hizo zimechangia kutatua changamoto zilizokuwa zikiwakabili walimu, kuongeza ari na morali ya kazi, pamoja na kuimarisha uwajibikaji na ufanisi katika kutekeleza majukumu yao.

"Tumekuwa tukishirikiana na ofisi nyingine zinazohusika kufuatilia changamoto za walimu na kuzitafutia ufumbuzi, hatua ambayo imesaidia kuboresha mazingira ya utendaji kazi na kuwawezesha walimu kuzingatia zaidi majukumu yao ya msingi," alisema Bw. Katyega.

Alifafanua kuwa utatuzi wa changamoto za walimu una mchango mkubwa katika kuboresha ufundishaji na ujifunzaji, kwani walimu wanapokuwa na utulivu wa kiakili na kisaikolojia huweza kujiandaa vizuri kwa masomo, kutumia mbinu bora za ufundishaji na kuwasaidia wanafunzi kuelewa masomo kwa ufanisi zaidi.

Katika hatua nyingine, Bw. Katyega alisema kuwa matumizi ya Mfumo wa Taarifa za Walimu (TSCMIS) yameboresha utendaji kazi na uwajibikaji kwa kurahisisha utoaji wa huduma, ikiwemo usajili wa walimu.

Alisema kuwa kupitia mfumo huo, Wilaya ya Nkasi ilisajili walimu 151 walioajiriwa katika kipindi cha mwaka 2024/2025, wakiwemo walimu 20 wa shule za msingi na 131 wa shule za sekondari.

Alieleza kuwa matumizi ya mifumo ya kidijitali ni miongoni mwa hatua zinazochangia kuboresha usimamizi wa taarifa za walimu, kurahisisha upatikanaji wa huduma na kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Tume.

Mafanikio hayo ni sehemu ya jitihada za Tume ya Utumishi wa Walimu za kuboresha huduma kwa walimu, kutatua changamoto zinazowakabili na kuimarisha usimamizi wa rasilimali watu katika sekta ya elimu.

WALIMU 230 KALAMBO WASAJILIWA KATIKA MFUMO WA TSCMIS

Na Mwandishi Wetu, Kalambo

Jumla ya walimu 230 katika Wilaya ya Kalambo, Mkoa wa Rukwa, wamesajiliwa katika Mfumo wa Taarifa za Walimu (TSCMIS), hatua inayochangia kuboresha usimamizi wa taarifa za walimu na kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma.

Hayo yameelezwa na Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Kalambo, Bw. Godfrey Kayonga, wakati wa mahojiano na Maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini kutoka Makao Makuu ya Tume, yaliyolenga kueleza mafanikio ya Tume katika kipindi cha miaka 10 tangu kuanzishwa kwake.

Akifafanua kuhusu usajili huo, Bw. Kayonga alisema kuwa walimu 119 ni wa shule za msingi, huku 111 wakiwa wa shule za sekondari.

Alisema kuwa matumizi ya mfumo huo yamerahisisha upatikanaji na uhifadhi wa taarifa za walimu kwa njia ya kidijitali, zikiwemo taarifa za ajira, upandishaji vyeo na vituo vya kazi.

"Mfumo huu umekuwa na mchango mkubwa katika usimamizi wa rasilimaliwatu katika sekta ya elimu. Umerahisisha utoaji wa huduma kwa walimu na kuongeza kasi, uwazi, ufanisi na uwajibikaji katika utekelezaji wa majukumu ya Tume," alisema Bw. Kayonga.

Aliongeza kuwa TSC Wilaya ya Kalambo imejipanga kuendelea kutoa elimu kwa walimu kuhusu matumizi sahihi ya mifumo ya kidijitali ili kuongeza uelewa wao na kuwawezesha kunufaika na huduma zinazotolewa kupitia mifumo hiyo.

Akizungumzia mabadiliko yaliyotokana na matumizi ya TSCMIS, Bw. Kayonga alisema kuwa mfumo huo umeimarisha usimamizi wa taarifa za walimu kwa kupunguza utegemezi wa nyaraka za karatasi na kurahisisha upatikanaji wa taarifa zinazohitajika katika utoaji wa huduma.



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Kalambo, Bw. Godfrey Kayonga, akieleza mafanikio ya Tume wakati wa mahojiano na Maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini kutoka Makao Makuu ya Tume.

Aidha, alisema kuwa katika kipindi cha mwaka 2023 hadi 2026, TSC Wilaya ya Kalambo imefanya ziara za usimamizi wa utendaji kazi na kutoa elimu kwa walimu kuhusu masuala ya ajira, maendeleo ya taaluma, maadili na nidhamu.

Alisema kuwa kupitia ziara hizo, jumla ya walimu 530 kutoka shule 42 walipatiwa elimu, wakiwemo walimu 413 wa shule za msingi na 117 wa shule za sekondari.

Kwa upande wake, Mwalimu Msafiri Ernest Ndwata aliipongeza TSC kwa kuendelea kuwa karibu na walimu kupitia ziara za kuwapatia elimu, kusikiliza changamoto zao na kusaidia kutafuta ufumbuzi wa kero zinazowakabili.

Alisema kuwa utaratibu huo umeongeza uelewa wa walimu kuhusu masuala mbalimbali ya kiutumishi na kutoa fursa ya changamoto zao kufanyiwa kazi.



Mwalimu Msafiri Ernest Ndwata akizungumza wakati wa mahojiano kuhusu huduma zinazotolewa na TSC Wilaya ya Kalambo.

Naye, Mwalimu Benard Twinzi Menard wa Shule ya Msingi Matai aliipongeza Serikali kwa hatua za kupandisha vyeo walimu kwa mserereko na kutatua changamoto za kiutumishi zilizokuwa zimewakabili kwa muda mrefu.

Alisema kuwa hatua hizo zimeongeza matumaini kwa walimu na kuonesha umuhimu wa kuendelea kuboresha huduma zinazotolewa kwa watumishi hao.

Mafanikio hayo ni sehemu ya juhudi za Tume ya Utumishi wa Walimu za kuboresha usimamizi wa taarifa za walimu, kuimarisha mawasiliano na wadau na kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma kwa walimu nchini.



Mwalimu Benard Twinzi Menard wa Shule ya Msingi Matai akieleza maoni yake kuhusu juhudi za Serikali katika kuboresha huduma kwa walimu.

WALIMU 552 SUMBAWANGA WAPANDISHWA VYEO KWA MSERERENKO

Na Mwandishi Wetu, TSC Sumbawanga

Jumla ya walimu 552 katika Wilaya ya Sumbawanga, Mkoa wa Rukwa, wamepandishwa vyeo kwa mserereko, hatua inayolenga kutatua changamoto za muda mrefu za kiutumishi na kuboresha ustawi wa walimu.

Hayo yameelezwa na Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Sumbawanga, Bw. Godfrey Michael Kisamo, wakati wa mahojiano na Maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini kutoka Makao Makuu ya Tume, yaliyolenga kueleza mafanikio ya Tume katika kipindi cha miaka 10 tangu kuanzishwa kwake mwaka 2016.

Akifafanua kuhusu upandishaji huo, Bw. Kisamo alisema kuwa walimu 376 wa shule za msingi na 176 wa shule za sekondari walinufaika na utaratibu huo, ambao umesaidia kushughulikia changamoto za upandishaji vyeo zilizokuwa zikiwakabili walimu.

Aidha, alisema kuwa katika kipindi cha mwaka 2023 hadi 2026, walimu 90 walibadilishiwa vyeo baada ya kukidhi vigezo vilivyowekwa kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu zinazosimamia utumishi wa walimu. Kati yao, 73 walikuwa wa shule za msingi na 17 wa shule za sekondari.

Katika hatua nyingine, Bw. Kisamo alisema kuwa katika kipindi hicho, walimu 271 walipata fursa ya kwenda masomoni kujiendeleza katika fani mbalimbali, ikiwa ni sehemu ya jitihada za kuongeza maarifa na ujuzi ili kuendana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia pamoja na mahitaji ya sekta ya elimu.

Aliongeza kuwa katika kipindi cha mwaka 2023 hadi 2026, jumla ya walimu 2,716 walipandishwa vyeo, wakiwemo 1,865 wa shule za msingi na 851 wa shule za sekondari.



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Sumbawanga, Bw. Godfrey Michael Kisamo, akifafanua mafanikio ya Tume wakati wa mahojiano ofisini kwake.

Kwa upande wake, Mwalimu Rahabu Langson Mwaijibe wa Shule ya Sekondari Kantalamba aliipongeza Tume ya Utumishi wa Walimu kwa kuboresha huduma kwa walimu, akisema kuwa kwa sasa wanapata haki zao za kiutumishi kwa wakati na changamoto zinazohusiana na upandishaji vyeo na mabadiliko ya miundo ya utumishi zinashughulikiwa kwa ufanisi zaidi.

Alisema kuwa hali hiyo ni tofauti na ilivyokuwa katika kipindi cha mwaka 2013 hadi 2014, ambapo walimu walikabiliwa na changamoto mbalimbali katika kupata haki zao za kiutumishi.



Mwalimu Rahabu Langson Mwaijibe wa Shule ya Sekondari Kantalamba akieleza maoni yake kuhusu huduma zinazotolewa na Tume ya Utumishi wa Walimu wakati wa mahojiano na Maafisa wa TSC kutoka Makao Makuu.

Naye Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Mwenge B, Bw. Euzebius Sixto Bandora, aliipongeza TSC kwa kuimarisha ushirikiano na walimu kupitia ziara za mara kwa mara shuleni, zinazolenga kusikiliza na kutatua changamoto zao pamoja na kutoa elimu kuhusu Sheria, Kanuni na Taratibu zinazosimamia utumishi wa walimu.

Alisema kuwa ziara hizo zimeongeza uelewa wa walimu kuhusu haki na wajibu wao na kuwapa fursa ya kuwasilisha changamoto zao kwa Tume ili zipatiwe ufumbuzi.

Mafanikio hayo yanaonesha jitihada za Tume ya Utumishi wa Walimu katika kuboresha usimamizi wa utumishi, kutatua changamoto za walimu na kuwawezesha kuzingatia zaidi majukumu yao ya msingi ya ufundishaji na ujifunzaji.



Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Mwenge B, Bw. Euzebius Sixto Bandora, akieleza mchango wa Tume ya Utumishi wa Walimu katika kutatua changamoto za walimu wakati wa mahojiano.

TSC YAHITIMISHA KIKAO KAZI CHA KUPITIA MAANDALIZI YA KANUNI ZA KUBORESHA HUDUMA KWA WALIMU

Na Mwandishi Wetu – Morogoro

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) imehitimisha kikao kazi cha kupitia na kutoa maoni kuhusu maandalizi ya kanuni zinazolenga kuboresha utoaji wa huduma kwa walimu nchini, huku washiriki wakisisitizwa kuhakikisha maoni yaliyotolewa yanachangia kuandaa kanuni zinazokidhi mahitaji ya sasa ya utumishi wa walimu.

Akizungumza wakati wa kufunga kikao kazi hicho tarehe 23 Oktoba 2026, Mkurugezi wa Kitengo cha Huduma za Sheria, Wakili Edwin Mgendera, aliwashukuru washiriki kwa ushiriki wao na mchango walioutoa katika mchakato wa kupitia maandalizi ya kanuni hizo.

Amesema kazi iliyofanyika ni muhimu sana katika kuhakikisha kanuni zitakazoandaliwa zinazingatia mahitaji ya sasa na kuweka msingi mzuri wa kuboresha utoaji wa huduma kwa walimu nchini.

Aidha, amesisitiza umuhimu wa kuzingatia maoni na mapendekezo yaliyotolewa wakati wa kikao hicho ili kusaidia kuandaa kanuni zitakazowezesha Tume kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi na kukidhi matarajio ya walimu wanaohudumiwa.

Kikao hicho ni sehemu ya juhudi za TSC kuendelea kuboresha mifumo ya kiutendaji na kisheria ili kuimarisha usimamizi wa Utumishi wa Walimu na kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma kwa walimu nchini.



Mkurugezi wa Kitengo cha Huduma za Sheria wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Wakili Edwin Mgendera, akitoa neno la kufunga kikao kazi cha kupitia na kutoa maoni kuhusu maandalizi ya kanuni za kuboresha utoaji wa huduma kwa walimu, tarehe 23 Oktoba, 2026 mjini Morogoro.









Washiriki wa kikao kazi cha kupitia na kutoa maoni kuhusu maandalizi ya kanuni za TSC wakifuatilia hotuba ya mgeni rasmi wakati wa kufunga kikao hicho, tarehe 23 Oktoba, 2026 mjini Morogoro.

TSC YAHITIMISHA KIKAO KAZI CHA KUPITIA MAANDALIZI YA KANUNI ZA KUBORESHA HUDUMA KWA WALIMU











Mkurugezi wa Kitengo cha Huduma za Sheria wa TSC, Wakili Edwin Mgendera (katikati), akiwa katika picha ya pamoja na washiriki wa kikao kazi cha kupitia na kutoa maoni kuhusu maandalizi ya kanuni za Tume, kilichohitimishwa tarehe 23 Oktoba 2026 mjini Morogoro.

TSC YAHITIMISHA KIKAO KAZI CHA KUPITIA MAANDALIZI YA KANUNI ZA KUBORESHA HUDUMA KWA WALIMU










KIKAO CHA KAMATI YA TEHAMA

















Kikao cha Kamati ya TEHAMA cha Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kikiendelea katika Ukumbi wa Ofisi ya Tume, Makao Makuu, jijini Dodoma. Kikao hicho kilifanyika tarehe 4 Novemba 2026.

KIKAO CHA KAMATI YA TEHAMA









Kikao cha Kamati ya TEHAMA cha Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kikiendelea katika Ukumbi wa Ofisi ya Tume, Makao Makuu, jijini Dodoma. Kikao hicho kilifanyika tarehe 4 Novemba 2026.

MAFUNZO KWA WAKUU WA SHULE YAIMARISHA USIMAMIZI WA SHERIA NA NIDHAMU MBARALI

Na Mwandishi Wetu, Mbalali

Mafunzo yanayotolewa na Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) katika Wilaya ya Mbalali, Mkoa wa Mbeya, yamechangia kuimarisha usimamizi wa maadili na nidhamu ya walimu pamoja na kuongeza uelewa wa Sheria, Kanuni na Taratibu za utumishi wa umma miongoni mwa viongozi wa shule.

Hayo yameelezwa na Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Mbalali, Bw. Andulile Mwangoka, wakati akieleza mafanikio ya Tume katika kipindi cha miaka 10 tangu kuanzishwa kwake mwaka 2016.

Bw. Mwangoka alisema kuwa mafunzo hayo yamelenga kuwajengea uwezo wakuu wa shule za msingi na sekondari pamoja na watumishi wa Tume katika kusimamia maadili, nidhamu na uwajibikaji wa walimu katika maeneo yao ya kazi.

Aliongeza kuwa Tume imeendelea kuimarisha usimamizi wa utumishi wa walimu kupitia ziara za mara kwa mara shuleni, vikao vya uhamasishaji na usambazaji wa machapisho yanayotoa elimu kuhusu Sheria, Kanuni na Taratibu za utumishi wa umma.

"Katika kipindi cha miaka 10, Tume imeendelea kutoa mafunzo kuhusu maadili na nidhamu kwa wakuu wa shule, kufanya ziara za usimamizi na kusambaza machapisho yanayohamasisha walimu kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za utumishi wa umma," alisema Bw. Mwangoka.

Akizungumzia ushirikishwaji wa walimu, alisema kuwa Tume imeimarisha utaratibu wa kupokea maoni na changamoto za walimu pamoja na wadau wengine kupitia mawasiliano ya ana kwa ana wanapofika ofisini, sanduku la maoni na Mfumo wa Taarifa za Walimu (TSCMIS).

Aidha, alisema kuwa Tume imeimarisha uchambuzi na uhakiki wa madai ya walimu kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya, ikiwemo kupitia majalada na kufuatilia hatua zinazopaswa kuchukuliwa ili kuwawezesha walimu kupata stahiki zao kwa wakati.

Kwa mujibu wa Bw. Mwangoka, jitihada hizo zimechangia kupunguza malalamiko yanayohusiana na upandishaji vyeo na mabadiliko ya miundo ya utumishi katika kada ya ualimu, hivyo kuwapa walimu utulivu zaidi katika kutekeleza majukumu yao.

Katika hatua nyingine, alisema kuwa matumizi ya mifumo ya kielektroniki yameimarisha usimamizi wa taarifa za walimu na kurahisisha ufuatiliaji wa changamoto mbalimbali za kiutumishi, ikiwemo masuala ya uhamisho wa vituo vya kazi.

Alifafanua kuwa Tume imeendelea kutoa maelekezo kwa walimu kuhusu taratibu za uhamisho na kushirikiana na ofisi zinazohusika katika kushughulikia changamoto zinazojitokeza.

Aliongeza kuwa elimu kuhusu maadili, nidhamu na taratibu za kiutumishi, ikiambatana na usimamizi wa karibu wa walimu, imechangia kuimarisha uwajibikaji na mwenendo wa walimu katika mazingira ya kazi.

Mafanikio hayo yanaonesha mchango wa Tume ya Utumishi wa Walimu katika kuimarisha usimamizi wa utumishi wa walimu, kuboresha huduma kwa walimu na kuweka mazingira yanayowawezesha kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za utumishi wa umma.



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Mbalali, Bw. Andulile Mwangoka (wa kwanza kulia) akiwa na watumishi wenzake wakati akieleza mafanikio ya Tume katika kipindi cha miaka 10 tangu kuanzishwa kwake mwaka 2016.



MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz